FUNZO LA 28

1. Je, kwa nini kichaka kilichokuwa kikiwaka moto alichokiona Musa hakikuharibiwa?
-Kwa sababu Mungu alikuwa ndani ya hicho kichaka.

2. Je, kwa nini Mungu alikuwa ndani ya kichaka kilichowaka moto?
-Kwa sababu Mungu alitaka kunena na Musa kuhusu Waisraeli.

3. Je, Waisraeli walikuwaje kama kichaka kilichowaka moto?
-Kama vile moto ulivyotaka kuharibu kichaka ndivyo Farao alivyojaribu kuharibu Israeli.
-Kama vile Mungu alivyokuwa ndani ya kichaka kilichowaka moto, ndivyo alivyokuwa na Waisraeli.

4. Je, jina "MIMI NIKO" linamaanisha nini?
-Linamaanisha kuwa Mungu hana mwanzo.
-Linamaanisha kuwa Mungu hana mwisho.
-Linamaanisha kuwa Mungu amekuwa hai wakati wote.
-Linamaanisha kuwa hakuna wakati ambapo Mungu hakuwepo.

5. Je, Mungu alijua kuwa Farao hangewaachilia Waisraeli kutoka Misri?
-Ndiyo.

6. Je, ishara ya kwanza ambayo Mungu alimpa Musa kuonyesha kuwa alimchagua Musa kuwaongoza Israeli kutoka Misri ilikuwa ipi?
-Fimbo ya Musa iligeuka kuwa nyoka, kisha ikarejea kuwa



fimbo.

7. Je, ishara ya pili ya kuonyesha kuwa Mungu alimchagua Musa kuwaongoza Israeli kutoka Misri ilikuwa ipi?
-Mkono wa Musa ulishikwa na ukoma alipoutia ndani ya koti yake na ukapona alipourejesha mara ya pili.

8. Je, Mungu alimtuma nani kumsaidia Musa kunena na Farao?
-Ndugu yake Musa Haruni.

9. Je, kwa nini Mungu alitaka kuwaokoa Israeli kutoka utumwa?
-Kwa sababu Mungu aliwapenda, hakutaka waishi katika utumwa.
-Kwa sababu Mungu alimuahidi Ibrahamu kuwa angewarejesha katika nchi ya Kanaani.
-Kwa sababu Mungu alimuahidi Ibrahamu kuwa angemtuma Mwokozi kupitia kwa Israeli.

-Mungu alitimiza ahadi yake kwa Musa kwa kumtuma ndugu yake Haruni amsaidie.

Tusome Kutoka 4:27-28

27-Bwana akamwambia Haruni, Nenda jangwani uonane na Musa. Naye akaenda, akamkuta katika mlima wa Mungu, akambusu.
28-Musa akamwambia Haruni hayo maneno yote ya Bwana ambayo alimtuma aende nayo, na ishara hizo zote alizomwagiza.

-Kisha Musa na Haruni walisafiri kwenda Misri.

-Musa na Haruni walipofika Misri, waliwakusanya Waisraeli pamoja kisha wakawaambia kile ambacho Mungu alimwambia Musa.

Tusome Kutoka 4:29-31

29-Musa na Haruni wakaenda, wakawakusanya wazee wote wa watu wa Israeli.
30-Haruni akawaambia maneno yote Bwana aliyonena na Musa akazifanya zile ishara mbele ya watu.
31-Watu wakaamini, na waliposikia ya kuwa Bwana amewajilia wana wa Israeli, na ya kuwa ameyaona mateso yao, wakainama vichwa vyao wakasujudu.

-Je, Waisraeli waliamini Neno la Mungu, kuwa Mungu alinena na Musa?
-Ndiyo.

-Je, ni kwa nini ilikuwa vizuri kwamba Waisraeli waliamini Neno la Mungu?

-Kwa sababu Mungu pekee ndiye angeweza kuwaokoa.

-Kwa sababu Neno la Mungu pekee ndilo lingeweza kuokoa Israeli.

-Je, ikiwa hatutaamini Neno la Mungu, tunamuitaje Mungu?
-Muongo.



-Je, Mungu atawaokoa wasioamini Maneno ya Mungu?
-La.

-Kama hatutaamini Maneno ya Mungu basi hatutaokoka.

-Mungu anataka usikilize Maneno yake ili uokoke.

-Mungu tu ndiye awezae kutuokoa.
-Ni Maneno ya Mungu tu yanayoweza kutuokoa.

-Baada ya Musa na Haruni kumaliza kuwaongelesha Waisraeli, walienda kuzungumza na Farao.

Tusome Kutoka 5:1-2

1-Hata baadaye, Musa na Haruni wakaenda wakamwambia Farao, wakasema, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Wape watu wangu ruhusa waende, ili kunifanyia sikukuu jangwani.
2-Farao akasema, Bwana ni nani, hata niisikilize sauti yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Mimi simjui Bwana, wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao.

-Farao alisema nini Musa alipomwambia kuwa Bwana amemwamuru awaachilie Waisraeli?

-Farao alisema “Simjui Bwana, na sitawaachilia Waisraeli.”

-Je, kwa nini Farao hakumjua Mungu?

-Kwa sababu Farao hakutaka kumjua Mungu.
-Kwa sababu Farao hakutaka kumwamini Mungu.

-Kwa sababu Farao alipenda dhambi yake.

-Farao na watuu wa Misri hawakumwamini Mungu.

-Farao na watu wake waliabudu mto mkubwa uliokuwa nchini mwao.

-Farao na watu wa Misri waliabudu jua, mwezi na nyota, pia wanyama wengi.

-Watu wa Misri pia walimuabudu Farao kama Mungu wao.

-Farao na watu wa Misri waliabudu kile ambacho Mungu aliumba badala ya kumwabudu Mungu.

-Wakati wa Farao, watu wengi walikataa kuamini ukweli wa Mungu.

-Pia sasa, watu wengi wamekataa kuamini ukweli wa Mungu.

-Kwa sababu watu wengi walikataa kuamini kweli za Mungu, Mungu alimruhusu Shetani awadanganye.

-Shetani akawadanganya watu, na wakaabudu kila kitu isipokuwa Mungu.

-Kwa sababu watu wengi walikataa kuamini ukweli wa Mungu,



Mungu alimchagua Ibrahamu awe baba wa Israeli.

-Mungu aliamua kumtuma Mwokozi kupitia kwa Ibrahamu na Waisraeli.

-Mungu pia aliamua kuandika kweli zake katika Kitabu chake, ambacho aliandika kupitia kwa Ibrahamu na Waisraeli.

-Kitabu cha Mungu kinaitwa Biblia.

-Je, Mungu alijua kuwa Farao hatawaruhusu Waisraeli watoke Misri?
-Ndiyo.

-Mungu anajua kila kitu kiatachofanyika kabla kifanyike.

-Baada ya Farao kukataa kuwaruhusu Waisraeli kwenda, sikiliza kile Mungu alimwambia Musa:

Tusome Kutoka 6:1

1-Bwana akamwambia Musa, Sasa utaona nitakavyomtenda Farao; maana kwa mkono hodari atawapa ruhusa kwenda zao, na kwa mkono hodari atawafukuza katika nchi yake.

-Je, kwa nini Mungu aliamua kuonyesha nguvu zake kuu kwa Farao na Wamisri?

-Ili wajue kuwa yeye pekee ndiye Mungu wa kweli.

-Mungu aliamua kumwonyesha Farao na Wamisri kuwa huo mto mkubwa katika nchi yao si Mungu.

-Mungu aliamua kumwonyesha Farao na Wamisri kuwa jua, mwezi na nyota si Mungu.

-Mungu aliamua Kumwonyesha Farao na Wamisri kuwa wanyama wao wengi si Mungu.

-Mungu aliamua kumwonyesha Farao na Wamisri kuwa Farao si Mungu.

-Mungu aliamua kuwaonyesha Waisraeli nguvu zake ili wajue kuwa yeye ni Mungu wao.

Tusome Kutoka 6:2-8

2-Kisha Mungu akasema na Musa, akamwambia, Mimi ni YEHOVA;

3-nami nilimtokea Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kama Mungu Mwenyezi, bali kwa jina langu YEHOVA sikujulikana kwao.

4-Tena nimelithibitisha agano langu nao, la kuwapa nchi ya Kanaani; nchi ya kukaa kwao hali ya ugeni.

5-Na zaidi ya hayo, nimesikia kuugua kwao wana wa Israeli, ambao Wamisri wanawatumikisha, nami nimelikumbuka agano langu.

6-Basi waambie wana wa Israeli, Mimi ni YEHOVA, nami nitawatoa ninyi mtoke chini ya mizigo ya Wamisri, nami nitawaokoa na utumwa wao, nami nitawakomboa kwa mkono



ulionyoshwa, na kwa hukumu kubwa;

7- nami nitawatwaeni kuwa watu wangu, nitakuwa Mungu kwenu; nanyi mtajua ya kuwa mimi ni YEHOVA, Mungu wenu, niwatoaye mtoke chini ya mizigo ya Wamisri.

8-Nami nitawaleta hata nchi ile ambayo naliinua mkono wangu, niwape Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo; nitawapa iwe urithi wenu; Mimi ni YEHOVA.

-Mungu aliamua kuonyesha nguvu zake kwa Waisraeli ili wajue kuwa yeye ni Mungu wa Ibrahamu, Isaka na Yakobo.

-Mungu aliamua kuonyesha nguvu zake kwa Waisraeli ili wajue kuwa yeye ni Mungu wao, Mungu wa Waisraeli.

-Kwa sababu Farao hakuwaruhusu Waisraeli kwenda, Mungu alimwonyesha nguvu zake kuu.

-Je, Mungu alionyeshaje nguvu zake kuu kwa Waisraeli na Wamisri?

-Mungu alituma mapigo makubwa kwa Farao na Wamisri.

-Katika pigo la kwanza, Mungu alibadilisha maji ya mto wao mkubwa kuwa damu.

-Ila hilo pigo, halikufika katika eneo ambalo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 7:20-21

20-Musa na Haruni wakafanya hivyo, kama Bwana

alivyowaambia; naye akaiinua ile fimbo, na kuyapiga maji yaliyokuwa mtoni, mbele ya Farao, mbele ya watumishi wake; na hayo maji yote yaliyokuwa katika mto yakageuzwa kuwa damu.

21-Hao samaki waliokuwa mtoni nao wakafa; na ule mto ukatoa uvundo, Wamisri wasipate kunywa maji ya mtoni; na ile damu ilikuwa katika nchi yote na Misri.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo, na akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwaruhusu Waisraeli waondoke.

-Kwa pigo la pili, Mungu alituma pigo la chura.

-Sehemu alioishi Farao na Wamisri ilijaa vyura.

-Ila hilo pigo, halikufika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 8:5-6

5-Bwana akamwambia Musa, Mwambie Haruni, Nyosha mkono wako na fimbo yako juu ya mito, juu ya vijito, na juu ya maziwa ya maji, ukawalete vyura waje juu ya nchi yote ya Misri.

6-Basi Haruni akaunyosha mkono wake juu ya maji yote ya Misri; na hao vyura wakakwea juu, wakaifunika nchi ya Misri.



-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo, na akasema kwamba atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa lile pigo, Farao alikataa kuwaruhusu Waisraeli kuondoka.

-Katika pigo la tatu, Mungu alituma chawa.

-Farao, Wamisri na pia nchi ya Wamisri ilijawa na chawa.

-Ila hilo pigo, halikufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 8:16-17

16-Bwana akamwambia Musa, Mwambie Haruni, Nyosha fimbo yako, ukayapige mavumbi ya nchi, ili kwamba yawe chawa katika nchi yote ya Misri.

17-Nao wakafanya; Haruni akaunyosha mkono wake na fimbo yake, na kuyapiga mavumbi ya nchi, nayo yakawa chawa juu ya wanadamu na juu ya wanyama; mavumbi yote ya nchi yakawa ni chawa katika nchi yote ya Misri.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo na akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwarusu Waisraeli kuondoka.

-Kwa pigo la nne, Mungu alituma pigo la nzi.

-Nchi ya Farao na Wamisri ilijawa na nzi.

-Ila hilo pigo, halikufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 8:24

24-Bwana akafanya; wakaja wingi wa mainzi kwa uzito sana, wakaingia nyumbani mwa Farao, na katika nyumba za watumishi wake, tena katika nchi yote ya Misri; nayo nchi iliharibiwa kwa ajili ya wale mainzi.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo, akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwarusu Waisraeli kuondoka.

-Kwa pigo la tano, Mungu alituma pigo la kuua wanyama wote.

-Farasi, ng'ombe, ngamia, punda, na kondoo wote wa Wamisri na wa Farao walikufa

-Ila hilo pigo, halikufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 9:6-7

6-Bwana akalifanya jambo hilo siku ya pili, na wanyama wote wa kufugwa wa Misri wakafa; lakini katika wanyama wa



wana wa Israeli hakufa hata mmoja.

7-Farao akatuma watu, na tazama, hapana mmoja aliyekufa katika wanyama wa wana wa Israeli. Lakini moyo wa Farao ulikuwa mzito, wala hakuwapa hao watu ruhusa waende zao.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo na akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwarusu Waisraeli kuondoka.

-Katika pigo la sita, Mungu alituma majipu.

-Farao na Wamisri wote walijawa na majipu.

-Ila hilo pigo, halikufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 9:10

10-Basi wakatwaa majivu ya tanuuni, na kusimama mbele ya Farao; na Musa akayarusha juu mbinguni nayo yakawa ni majipu yenye kufura na kutumbuka juu ya wanadamu na juu ya wanyama.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo na akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwarusu

Waisraeli kuondoka.

-Katika pigo la saba, Mungu alituma mvua ya mawe.

-Mvua ya mawe ilinyesha katika nchi ya Misri, ikaharibu miti na mimea ya Wamisri na ya Farao.

-Ila hilo pigo, halikufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 9:23-26

23-Musa akaunyosha mkono wake kuelekea mbinguni; na Bwana akaleta ngurumo na mvua ya mawe, na moto ukashuka juu ya nchi; Bwana akanyesha mvua ya mawe juu ya nchi yote ya Misri.
24-Basi palikuwa na mvua ya mawe, na moto uliochanganyikana na ile mvua ya mawe, nzito sana, ambayo mfano wake haukuwapo katika nchi yote ya Misri tangu ilipoanza kuwa taifa.
25-Na ile mvua ya mawe ikapiga kila kilichokuwako mashambani, binadamu na mnyama, katika nchi yote ya Misri; hiyo mvua ya mawe ikapiga kila mmea wa mashambani, na kuuvunja kila mti wa mashamba.
26-Katika nchi ya Gosheni peke yake, walikokaa wana wa Israeli, haikuwako mvua ya mawe.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo na akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.



-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwarusu Waisraeli kuondoka.

-Katika pigo la nane, Mungu alituma pigo la nzige.

-Nzige walikula miti na mimea ya Wamisri na Farao iliyobaki.

-Ila hilo pigo, halikufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 10:13-15

13-Basi Musa akainyosha fimbo yake juu ya nchi ya Misri, na Bwana akaleta upepo kutoka mashariki juu ya nchi, mchana kutwa, na usiku kucha; kulipopambazuka ule upepo wa mashariki ukawaleta nzige.
14-Na hao nzige wakakwea juu ya nchi yote ya Misri, wakatua ndani ya mipaka yote ya Misri, walikuwa wabaya mno; hawajakuwapo nzige kama hao majira yo yote, wala baada yao hawatakuwa wengine jinsi hiyo.
15-Kwa sababu waliufunika uso wote wa nchi, hata nchi iliingia giza; wakala mimea yote ya nchi, na matunda yote ya miti yaliyosazwa na ile mvua ya mawe; hapakusalia hata jani moja, mti wala mmea wa mashamba, katika nchi yote ya Misri.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo na akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwaruhusu Waisraeli kuondoka.

-Katika pigo la tisa, Mungu alituma pigo la giza.

-Giza lilifunika nchi ya Farao na Wamisri kwa siku tatu nzima.

-Ila hilo pigo, halikufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi.

Tusome Kutoka 10:21-23

21-Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako kuelekea mbinguni, kuwe giza juu ya nchi ya Misri, watu wapapase-papase gizani.
22-Basi Musa akaunyosha mkono wake kuelekea mbinguni; kukawa na giza nene katika nchi yote ya Misri muda wa siku tatu;
23-hawakupata kuonana mtu na mwenziwe, wala hakuondoka mtu mahali alipokuwa muda wa siku tatu; lakini wana wa Israeli wote walikuwa na mwanga makaoni mwao.

-Farao alimwomba Musa aondoe hilo pigo na akasema kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.

-Lakini Mungu alipoondoa hilo pigo, Farao alikataa kuwarusu Waisraeli kuondoka.

-Je, Farao alisema nini kila wakati Mungu alipotuma pigo?

-Farao alimwambia Musa kuwa atawaruhusu Waisraeli waondoke.



-Je, Farao alifanya nini kila wakati Mungu alipoondoa pigo?
-Farao alikataa kuwaruhusu Waisraeli waondoke.

-Je, kwa nini mapigo hayakufika katika sehemu ambayo Waisraeli waliishi?

-Kwa sababu Mungu aliahidi Ibrahamu, Isaka na Yakobo kuwa atawabariki na kuwafanya kuwa watu wengi.

-Kwa sababu Mungu alikuwa akionyesha Farao, Wamisri na Waisraeli kuwa yeye ndiye Mungu pekee na hakuna mwingine.

-Hata baada ya haya mapigo makali, Farao alikataa kuwaruhusu Waisraeli kuondoka.

-Hata baada ya haya mapigo makali, Farao alikataa kumtii Mungu.

-Je, Farao anaweza pigana dhidi ya Mungu na ashinde?
-La.

-Je, yeyote anaweza pigana dhidi ya Mungu na ashinde?
-La.

-Je, nini kitakachowafanyikia wale wanaopigana dhidi ya Mungu?
-Mungu atawaharibu.

-Kataika fundisho lifuatalo, tutajifunza kuhusu pigo la mwisho.